BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini – Tarehe 03 Juni, 2025
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

302. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni kwa kiasi gani Serikali imedhibiti Taasisi Zisizo za Kiserikali (NGOs) zinazotumika kuhamasisha uvunjifu wa amani kwa kutumia kivuli cha utoaji wa elimu ya mpiga kura katika vipindi kama hivi vya uchaguzi.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

296. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Dhana ya ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ni nzuri kwa vile inaharakisha maendeleo ya nchi na kukuza sekta zote. Lakini kwa muda sasa wawekezaji binafsi hawana uwezo wa kutosha wa kushindana na wawekezaji wanaotoka nje katika kupata miradi mbali mbali.

Je, Wizara ina mpango gani katika kuhakikisha wawekezaji wa ndani wanalindwa na kunufaika na ushirikiano huu wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma pasipo kumezwa na kampuni kubwa kutoka nje kwa miradi wanayoimudu kuitekeleza.

64. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliweka maeneo tengefu kwa ajili ya uwekezaji kwa muda mrefu sasa.

Je, kuna utaratibu gani wa uendelezaji wa maeneo hayo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

41. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Wafanyakazi wengi wa Serikali wanalalamika juu ya kodi ya mapato katika mishahara ya wafanyakazi (PAYE) wanayokatwa katika mishahara yao. Ukubwa wa kodi hii umepunguza uwezo wa wafanyakazi wengi kuweza kujikimu kimaisha kutokana na kupanda kwa gharama za maisha.

(a) Je, Serikali inalitambua vipi tatizo hili la ukubwa wa kodi ya PAYE.

(b) Je, kwa mshahara wa kiwango cha chini mfanyakazi hutakiwa kulipa kodi ya PAYE kiasi gani.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha hukusanywa kwa mwezi kutokana na kodi ya PAYE.

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kiasi gani Serikali inakabiliana na changamoto ya ufinyu wa elimu ya kifedha katika jamii.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

109. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tathmini iko vipi juu ya idadi ya uwepo wa Wakalimani wa Lugha za Alama kwa muktadha wa mahitaji ya jamii.

201. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamatuni na Michezo:

Tathmini ya vipindi pendwa kwa sasa ipo vipi katika mabadiliko ya ubora wa vipindi kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC).

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

129. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa hiliki, mdalasini na pilipili manga zinatumika sana Zanzibar, na kwa kuwa kuna haja ya kuwaelimisha zaidi wananchi kulima kilimo hiki na kupata tija.

Je, utafiti uko vipi kwa wale waliolima na wamepata mafanikio yepi ya kuwahamasisha wanachi wengine waweze kulima kilimo hiki.

192. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wengi wamejitokeza kujiajiri kwenye kilimo cha bustani za kupendezesha nyumba, miji na mitaa mbali mbali.

(a) Kwa kiasi gani na vipi wananchi hawa wanapata mashirikiano kutoka Serikalini.

(b) Serikali inatumia utaratibu gani wa kuwapatia maeneo katika kandokando ya barabara ili kuweza kuupendezesha mji wetu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

173. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali ipo katika hatua gani kwa sasa katika jitihada zake za kuwa na vyanzo vya umeme vya uhakika.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

254. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Natambua uwekezaji wa kimifumo na usimamizi wa Shirika la Bandari la Zanzibar.

Je, kuna utofauti upi wa kiufanisi na kimapato kwa Shirika la Bandari kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

239. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi walioathirika na ujenzi wa barabara ya Kitogani hadi Paje wanamadai ya kulipwa fidia za nyumba zao pamoja na mazao yao kutokana na kupisha ujenzi wa barabara unaoendelea.

(a) Je, Wizara yako ina ufahamu upi wa tatizo hili.

(b) Ni lini wananchi hao watalipwa fidia zao.

(c) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananachi hao.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

250. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, Serikali imefanya tathmini ipi kujua takwimu ya vyombo vya uvuvi na wavuvi hapa Zanzibar.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

229. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwa vipi dhamira ya mabadiliko ya Mtaala Mpya inaweza kutatua changamoto za mahitaji ya kiufundi na rasilimali watu kwa miradi mbali mbali ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa.

285. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha za kujikimu na ada (maarufu boom) kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu wenye kupata ufadhili wa Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar.

Ni ipi sababu na hatua zilizochukuliwa na Wizara yako kutatua changamoto hii.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

13. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katikati ya msitu wa Ngezi liko bango moja linaloonesha uwepo wa makaburi ya Mashekhe wenye asili ya Kiajemi waliozikwa hapo lakini hapana kiashiria maalum cha jengo wala kaburi lenyewe la watu hawa muhimu wenye historia kubwa.

(a) Kwa nini Serikali haioni haja ya kuyajengea makaburi haya pamoja na kuitafuta historia ya Mashekhe hawa na kuandika kitabu cha historia yao.

(b) Kwa nini Serikali haiyatangazi makaburi haya ili kuvutia watalii wengi kutoka nchi za kiarabu na uajemi ili kujiongezea mapato yake.

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni nani Tip Tipp katika kumbukumbu za urithi wa utamaduni wa Mzanzibari.

(b) Ni upi mchango wake katika maandiko ya historia ya nchi yetu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**03 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**